JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE
SHULE YA SEKONDARI NYABIYONZA
S.L.P 74, KARAGWE, KAGERA, TANZANIA


Simu Mkuu wa shule 255(0)767 388 964/ 0624 728 659
Makamu mkuu wa shule 0766 748 534
Matroni 0624 935 402
Patroni 0769 776 535

Email: *nyabiyonzasec@gmail.com*


Ofisi ya Mkuu wa shule,
Shule ya sekondari Nyabiyonza,
S.L.P 74,
35413 – Kibondo
KARAGWE.

Tarehe 12/06/2023.

Jina la Mwanafunzi ……………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
S.L.P……………………………………………………………………………………

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYABIYONZA HALMASHAURI WILAYA YA KARAGWE MKOA WA KAGERA MWAKA 2023/2024.

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukutarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2023/2024 Tahasusi ya ……………………………… Shule ya sekondari Nyabiyonza ipo umbali wa KM 1 mashariki mwa mji wa Nyakaiga uliopo Kata ya Kibondo Wilayani Karagwe (**Kutoka stendi ya omurushaka kufika Nyakaiga nauli ni shilingi 5000 kwa Tax, na kutoka Nyakaiga kufika shuleni kwa usafiri wa pikipiki ni Tsh 1,500.**) Muhula wa kuanza masomo utaanza tarehe14/08/2023 unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023.

2.0 Michango mbalimbali

(a)

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule Na.31910024088 katika Bank ya NMB.
Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye Pay slip.

ANGALIZO: Jumla ya michango kwa wanafunzi wa bweni ni shilingi 80,000/= kwa mwaka.

(b) Mahitaji ambayo mwanayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni -:

3.0 Sare ya shule

3.1 WAVULANA

i. Suruali mbili za Blue bahari zenye urefu wa kufunika kisigino pasipo kuikanyaga na zenye malinda mawili kila upande, ziwe na mifuko miwili ya kawaida pembeni pia ziwe na mfuko mmoja nyuma wenye kishikizo. Mapana kwa chini (Yaani miguuni) iwe na vipimo vya inchi 16 -18 (Zisiwe za mitumba) Suruali itapimwa kuthibitisha vipimo.
ii. Aje na mashati mawili meupe ya mikono mirefu Aina ya (Tetroni). Yenye mfuko mmoja upande wa kushoto (yasiwe ya mitumba).
iii. Mkanda mweusi wa Ngozi upana usiozidi nchi mbili.
iv. Aje na jozi mbili za Viatu vyeusi vya Ngozi vya kufunga na Kamba visiwe Mabuti na visigino vyake viwe vifupi.
v. T- shirt 2 Bluu za kushindia (Adidas/ Sports)
vi. Soksi nyeusi jozi mbili au Zaidi, tai moja ya bluu Bahari (Zinapitikana shuleni).
vii. Aje na suruari za Kitambaa mbili Rangi ya Damu ya mzee kwa ajili ya kushindia. (Sifa ya suruali hizi iwe sawa na kifungu (i) hapo juu.

3.2. WASICHANA

i. Sketi 2 za Bluu bahari Linda box kubwa mbele na linda jingine kubwa nyuma na pembeni malinda mdogo matatu pande zote mbili **(Mshono wa masista).** Na upana wamkanda usiozidi nchi mbili (Lazima sketi iwe na nchi sita chini ya magoti). Na kitambaa kiwe original.
ii. Aje na mashati mawili meupe ya mikono mirefu Aina ya (Tetroni). Yenye mfuko mmoja upande wa kushoto (yasiwe ya mitumba).
iii. Aje na jozi mbili za Viatu vyeusi vya Ngozi vya kufunga na Kamba visiwe Mabuti na visigino vyake viwe vifupi.
iv. Soksi nyeupe jozi mbili au Zaidi tai moja ya bluu Bahari (Zinapitikana shuleni).
v.
vi. Rangi ya hijabu (suruali kwa wasichana) ifanane na sare ya shule jarabibi nyeupe mbili
vii. Nywele kichwani zisizidi sentimeta moja.
viii. Gauni mbili rangi ya Violet red (Damu ya mzee) za kushindia

3.3. SARE KWA WOTE

- Sweta ya shule rangi ya bluu
- Tisheti nzito rangi ya bluu yenye kora.
- Nywele fupi zisizozidi sentimeta moja, kusuka, kuweka dawa ya nywele au kunyoa kipara haviruhusiwi pia kubadili rangi ya Ngozi na kucha, Bangili, Heleni,Pete na vitu vingine haviruhusiwi

4.0: Nguo za michezo:

Aje na Track suit Rangi ya bluu na viatu vya raba.

CamScanner

## 4:1 VIFAA VYA KITAALUMA.

Unatakiwa uje na vifaa vya kutosha katika shughuli za masomo darasani:-

- Kalamu za wino na za risasi za kutosha.
- Kasha la vifaa vya hesabu. (Mathematical set)
- Rula
- Madaftari makubwa (Counter Books 12-Quire 3).
- Ream ya karatasi nyeupe 1 A4. Kwa kila muhula.
- File moja la kawaida kwa ajili ya kutunza mitihani yako.
- Kamusi ya kiingereza (Oxford Advanced Learner's Dictionary)
- Scientific calculator non programmable (CASIO fx – 991MS (Kwa wanaosoma tahasusi ya CBG na HGL)
- Dissecting kit kwa mwanafunzi wa Biology tu.
- Vitabu vya somo la tahasusi ulilochaguliwa kusoma, kwa somo la GEOGRAFIA vitabu vinavyo hitajika ni Physical Geograph (Msabila) Human and economic Geography practical (Zists kamili.)
- Kwa somo la BIOLOJIA aje na vitabu vya (TIE) for advanced level secondary school. Form V&VI. Lugha na sarufi na fasihi.
- Kwa somo la KISWAHILI aje na vitabu vya (TIE) Kiswahili kidato cha V&VI
- Kwa somo la HISTORIA aje na vitabu vya (TIE) History for advanced level secondary school Form V.
- Kwa somo la ENGLISH LANGUAGE Aje na vitabu vya English for advanced secondary school form V (TIE).
- Kwa somo la CHEMISTRY aje na vitabu vya Organic chemistry for advanced level secondary school (TIE) na General Chemistry advanced level secondary school (TIE).
- Kwa somo la MATHEMATICS aje na Basic Applied Mathematics (TIE)

### 4.2: VIFAA VYA KAZI

Unatakiwa kuja na vifaa vya kazi kwa ajili ya kutunza mazingira na shughuli za uzalishaji mali ambazo ni:-

Ndoo mbili ndogo (Lita kumi) za plastic zenye mifuniko, siko 1, Jembe1, Reki1, mifagio 2 wa ndani nan je.

### 4.3: MALAZI:

i. Godoro moja la sponge size futi 2 na nusu kwa sita ($2^1/_2$ x6)
ii. Mashuka mawili rangi ya pinki, Blanketi 1, mto na foronya ya pinki, chandarua 1
iii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe
iv. Kandambili jozi 1 za kuogea
v. Taulo.
vi. Nguo za ndani za kutosha kwa wote
vii. Sabuni za kufulia na kuogea,
viii. Mafuta ya kujipaka,ya mgando (siyo vipodozi wala lotion)
ix. Mswaki na dawa ya meno na Toilets papers 6.
x. Pedi pacti 5 kwa wasichana kwa muhula
xi. Aje na pesa kidogo kwa ajili ya kujikimu
xii. Tochi na betri zake (Kwa tahadhari)
xiii. Brashi ya kung'arisha viatu.
xiv. Viatu vya wazi (Open shoes) vya kushindia visiwe na visigino virefu
xv. Aje na passport size nne akiwa amevaa shati jeupe kitambaa cha nyuma kiwe cha bluu.

CamScanner

4.4: KUFIKA SHULENI/ SIKU YA KURIPOTI SHULENI

- Mwanafunzi anatakiwa kufika hapa shuleni tarehe 13/08/2023 saa 2:00 asubuhi. Mara afikapo shuleni aripoti moja kwa moja Ofisi kwa mkuu wa shule akiwa na mahitaji yote ya shule na mahitaji yote ya shule aliyojulishwa hapo juu tayari kwa kukaguliwa. Akichelewa kuripoti Zaidi ya wiki mbili bila sababu maalumu baada ya shule kufunguliwa atapoteza nafasi yake.
- Siku ya kuripoti ni Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:30 Alasiri (Muda wa kazi)
- **Kila mwanafunzi aje amevaa sare ya shule**

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Angalizo

1. Ili kuepukana na usumbufu wa kurudishwa nyumbani kutokana na kutotimiza mahitaji, unashauriwa kukamilisha mahitaji haya kabla ya kuripoti shuleni
2. USAFIRI: Itabidi ajigharamie kwa usafiri wa kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo
3. CHETI KUTOKA KWA DACTARI: Itabidi arudishe fomu iliyoambatanishwa ikiwa imethibitishwa na daktari wa Hospitali ya serikali ya Halmashauri ya wilaya au ya mkoa ya mkoa kuwa umepimwa na kwamba anaweza kumudu masomo na kazi za nje bili matatizo
4. Aje na RESULT SLIP yake ya kidato cha Nne. (Orignal na copy moja).
5. Uraia: Anatakiwa kuleta shuleni copy ya CHETI CHA KUZALIWA (Birth certificate)
6. KUKUBALI MASHARTI YA SHULE: Sheria za shule na fomu ya kukubali kutii kwa dhati sheria hizo pamoja na maelezo yako binafsi vimeambatanishwa Mwanafunzi azisome kwa makini sheria hizo, akizikubali, aweke Saini yake kwenye fomu ya kukubali kuijiunga mbele yako mzazi au mlezi. Pia ajaze fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi na aziwasilishe fomu hizo shuleni siku ya kuripoti
7. Abandike picha nne (4) za wazazi au ndugu wa karibu pamoja nan amba zao za simu wanazoweza kumtembelea mwanafunzi na kushirikiana ns shule katika mlezi.
8. Aje na bima ya afya ya mwanafunzi inayotolewa na NFIF (Shirika la Baima ya afya ya Taifa).

- Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA NYABIYONZA SEKONDARI.

THE HEADMASTER NYABIYONZA SEC SCHOOL P.O BOX 74, KARAGWE

RAPHAEL FELECIAN KILENZI
MKUU WA SHULE.

CamScanner

### 4.5:Sheria na Kanuni Muhimu za Shule.

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995.Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini chini ya ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji Elimu .Unatakiwa kunzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Kila mwanafunzi ni lazima kuvaa nguo za shule (School uniform), wakati wote awapo shuleni, na mahali pengine atakapotakiwa kufanya hivyo.

(b) Vitendo vya kushiriki au kushawishi mgomo wa aina yoyote shuleni ni marufuku kabisa

(c) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;

(d) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;

(e) Kushiriki kwa makini kufanya maandalizi ya jioni (preparations);

(f) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;

(g) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo; ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

(h) Ni muhimu kwa mwanafunzi Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule; (Usifuge ndevu, nywele ndefu kucha nk.)

(i) Ugomvi au kupigana, kuleta fujo madarasani, lughaza matusi, kashfa kwa mwenzako au wananchi ni mwiko kabisa.

(j) Kila mwanafunzi lazima aepuke na kuchukia vitendo vyovyote vya uongo, uzushi, wizi, uasherati, ulevi, uvutaji sigara, bangi Madawa ya kulevya na rushwa.

(k) Vipindi vyote vilivyoko kwenye ratiba lazima vihudhuriwe bila kukosa pamoja na shughuli za nje ya darasa

(l) Makoti, Vibandiko, Vizibao, kofia, kandambili, viatu vya wazi,mikanda mipana haviruhusiwi kamwe kuvaliwa wakati mwanafunziawapo ndani ya vazi la shule.

(m) Lugha inayotumika hapa shuleni ni kiingereza tu.

o. Ni marufuku kuwa na simu ya mkononi (Mobile Phone), Chip (line), Earphone/ Headphone, charger, power bank, kompyuta (Laptop), I pad, pasi ya umeme, Redio, Kondomu n.k. USIJE NAVYO SHULENI.

p. Ni marufuku kupeleka chakula mabwenini.

q. Ni marufuku kumiliki kifaa chochote kinachoweza kusaidia kufanya biashara yoyote mwanafunzi awapo shuleni. Mfano Kamera, kuuza vyakula au vinywaji n.k.

CamScanner

5. Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa Shule mara moja.

(a) Wizi.

(b) Uasherati na ushoga.

(c) Ubakaji.

(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.

(e) Kupigana au kupiga.

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

(g) Kudharau Bendera ya Taifa.

(h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba.

(i) Kuoa au kuolewa.

(j) Kutoa mimba.

(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

(l) Kukataa adhabu kwa makusudi.

(m) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

(n) Kujaribu jaribio lolote la kujiua kama kunywa sumu n.k.

(o) Kupanga/ kuishi mitaani ukiwa shuleni/wakati wa masomo

(p) Kutenda tendo lolote lisilokuwa la kawaida shuleni au nje ya shule.

**4.0 Mambo mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa shuleni na mwanafunzi**

(a) *"Medical Examination form"* ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali.Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya wanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tahadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**MASHARTI MENGINE**

Mwanafunzi akifanya uharibifu wa maksudi au kwa uzembe katika miundombinu iliyoainishwa hapo chini atawajibika kurejesha miundombinu hiyo katika hali yake ka kawaidapamoja nah atua zingine za kinidhamu kuchukuliwa dhidi yake

- Uharibifu wa miundombinu ya umeme. Mfano: kuchubua nyaya za umeme ili kuchaji simu, kuchemsha maji/chai n.k.
- Uharibifu wa miundombinu yam aji. Mfano kuharibu tepu za bomba la maji n.k.
- Uharibifu wa miundombinu ya majengo. Mfano kupasua vioo, kuchafua kuta, kuharibu vigae n.k.
- Uharibifu wa miundombinu ya vyoo. Mfano kuweka vitu vigumu (Mawe, vipande vya magodoro, karatasi, nguo n.k) kwenye matundu ya vyoo vya maji.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYABIYONZA.

……………………

RAPHAEL FELECIAN MUCHUTI KILENZI

MKUU WA SHULE.

CamScanner

KIAMBATISHO "A"

Anwani .............................
.........................................
.........................................
Tarehe .............................

Mkuu wa shule,
Shule ya sekondari Nyabiyonza,
Ss.l.p 74,
Karagwe – kagera

**YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYABIYONZA**

Mimi ........................................................................... kutoka ....................................
Nimepokea barua ya kuchaguliwa kujiunga na kidato cha TANO katika shule ya sekondari Nyabiyonza kuanzia mwaka ......................
Nakubali/ sikubali nafasi hiyo. Nimesoma na kuelewa sheria na masharti ya kujiunga na shule hii yaliyoambatanishwa. Hivyo Ninaahidi kwamba nitatimiza wajibu wangu nikiwa mwanafunzi kadri ya uwezo wangu wote na kwamba nimezisoma na kuzielewa sheria za shule , nitafuata sheria na kanuni zote za shule zilizopo na zitakazowekwa na mamlaka /ungozi wa shule/serikali.Aidha, nitafuata na kuzingatia miongozo na maelekezo mbalimbali ya shule /serikali yatakavyotolewa dhidi yangu.
nitakuwa na nidhamu nzuri na maadili mema wakati wote wa masomo na baada ya saa za masomo, ndani na nje ya mipaka ya shule kwa kipindi chote cha uanafunzi wangu. Endapo nitashindwa utii na kufuata sheria hizo hatua zinazostahili zichukuliwe dhidi yangu. Natoa ahadi hizi mbele ya mzazi/ mlezi wangu, ambaye naye ametia sahihi yake kifungu kinachofuata hapa
Saini ya mwanafunzi. ...................... Tarehe ...................

**SEHEMU YA II- MZAZI / MLEZI**

Mimi ........................................................ Mzazi /Mlezi wa
......................................................... Nakubali/ sikubali mtoto wangu ajiunge na shule ya sekondari Nyabiyonza Naahidi kutoa ushirikiano wa hali ya juu katika malezi bora kama vile kumpatia mwanafunzi mahitaji ya shule kwa wakati ili aweze kumudu masomo yake kama ilivyotegemewa.Aidha, nakili kukubaliana na kanuni na maelekezo mengine yaliyotolewa na yatakayotolewa na shule.
Naahidi kwamba, nitapokea na kutekeleza maelekezo/ maagizo mengine yatakayo tolewa na shule katika harakati za kumlea mwanangu katika maadili mema ya kitanzania.Aidha, nitahudhuria mikutano/vikao vyote vilivyoamuliwa kisheria ili kupata fursa ya kujua maendeleo ya shule na ya mwanangu kitaaluma na kitabia (mwenendo).
Nitakuwa tayari kutoa ushirikiano wa kutosha kwa viongozi wa shule katika mustakabali wa kumfunza na kumlea mwanangu muda wote awapo masomoni hapa shuleni, Ujuaji na uvurugaji itakuwa mwiko kwangu
Taarifa na mawasiliano yote yahusuyo mwanangu yatumwe kwa kutumia anwani ifuatayo
......................................................Namba za simu (i) Baba .........................
(ii) Mama ............................... (iii)Kaka /dada ......................................
(iv) Ndugu wa karibu ...............................
Mabadiliko yoyote ya anwani yangu nitayatumwa kwa mkuu wa shule kwa maandishi
Sahihi ya mzazi .................................. Tarehe ....................

** Futa lisilohusika*

KIAMBATISHO "B"
MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi ............................................................................ (Kama ilivyo kwenye form Four SEL Form na Birth certificate)
2. Tarehe ya kuzaliwa ....................................................
3. Anwani ya nyumbani ...................................................................
Mahali unapoishi (Nyumbani kwenu): Wilaya ...................... Tarafa ......................
Kata ......................... Kijij/mtaa .........................
4. Shule ya sekondari ulikotoka ...............................................................
Anwani .............................................................................................................
.......................................................................................................................
5. Dini ..............................................................................
6. Kabila ........................................................................
7. Taifa (*Mtanzania/ si mtanzania*) ....................................................

| |
|---|
| Picha ya baba mzazi |

Jina la Mama: ....................................................
Anwani ....................................Na. Simu (1).......................
Anaishi/ Haishi......................... (2) ..................................
Kazi yake.............................................................................

| |
|---|
| Picha ya mama mzazi |

Jina la Baba: : ....................................................
Anwani ....................................Na. Simu (1).......................
Anaishi/ Haishi......................... (2) ..................................
Kazi yake..................................................................................

| |
|---|
| Picha ya mlezi/ ndug wa karibu |

Jina la mlezi : ....................................................
Anwani ....................................Na. Simu (1).......................
Anaishi/ Haishi......................... (2) ..................................
Kazi yake.............................................................................

| |
|---|
| Picha ya mlezi/ ndug wa karibu |

Jina la mlezi: ....................................................
Anwani ....................................Na. Simu (1).......................
Anaishi/ Haishi......................... (2) ..................................
Kazi yake.............................................................................

Mimi ..............................................(Mwanafunzi) nathibitisha kuwa taarifa nilizojaza ni za kweli.

........................ ........................

*Sahihi ya mwanafunzi* *Tarehe*

Mimi ................................. (Mzazi /Mlezi) wa mwanafunzi .................................. nimehakikisha kuwa taarifa zilizojazwa hapo juu ni za kweli.

................................ ................................

❖ Jina la Afisa mtendaji wa Kijiji/Mtaa ..................................................
Sahihi ya Afisa mtendaji wa Kijiji/mtaa ........................... Tarehe .......................
Simu Na. 1......................... 2. ............................ 3. ..................................

KIAMBATISHO C

KARAGWE DISTRICT COUNCIL.

Nyabiyonza secondary school,
P.o.box 74,
Karagwe – kagera
Date ………………
To Medical Officer,
…………………………………
…………………………………
…………………………………
…………………………………

Ref: ……………………………………………………….(Name of student) I lease examine the named student as per Medical examination from below:

…………………………
HEADMASTER

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by Government Medical Officer)

Full name ………………………………………………………………………………

Age ………………….. Height ………………….. (cm) Weight ……………… (kg)

1. Blood count ……………………………………………………………………
2. Stool Examination ……………………………………………………………
3. Urinary………………………………………………………………………
4. STDs and other V.D ……………………………………………………………
5. T.B. and leprosy test ……………………………………………………………
6. Eye test ………………………………………………………………………
7. Ear test ………………………………………………………………………
8. Chest …………………………………………………………………………
9. Abdomen ……………………………………………………………………
10. Spleen ………………………………………………………………………
11. Pregnancy test ………………………………………………………………

Any additional information: E.g. Physical defects or impairments, infections, chronic or family diseass (eg. Sickle cell), in ability of eat certain foods etc.
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………

I have examined the above named student and I certify that he/she is FIT/ NOT FIT to pursue Secondary Educatiion

……………………………………… ……………………………
Date

Signature and official stamp

Station ……………………………… Designation ……………………